

Je, kuna madhara yoyote yanayompata kijana Albino wa kike au wa kiume anayeamua kutoanza kujamiiana hadi afikie umri uliokubalika?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ukweli ni kwamba hakuna athari zinazojulikana kwakusubiri au kuacha kujamiiana hadi mtu afikie umri unaokubalika / utu uzima au hata muda mrefu zaidi. Pia via vya uzazi havitaathirika kwa njia moja au nyingine (havisinyai wala kutoweka.) Kuna uvumi potofu unaodai kuwa watu wanaoacha kujamiiana kwa muda mrefu wanaota chunusi na upele usoni au pia kwenye sehemu zao za siri na wengine kuchanganyikiwa. Hakuna ukweli wowote kuhusu uvumi huu. Kuwa na chunusi usoni ni mojawapo ya hali inayowakabili vijana wenye umri kati ya miaka 13 hadi 19. Hali ya kuota chunusi inasababishwa na kuwepo mafuta mengi kwenye ngozi. Hali hii hubadilika kadiri umri unavyosogea mbele. Mara nyingi inashauriwa kufanya mazoezi ya mwili ili kuwezesha vitundu vilivyopo kwenye ngozi kufunguka na kuwezesha ngozi kupumua. Hakuna madhara ya kiafya ambayo yanatokana na kuacha kujamiiana, bali kinyume ni kuwa, kuna madhara mengi ya kiafya, hisia na ya kimwili yanayotokana na kujamiiana katika umri mdogo kama vile mimba zisizotarajiwa, uambukizo wa magonjwa yatokanayo na kujamiiana pamoja na Virusi vya UKIMWI.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25527>